## I: UTANGULIZI

Wilaya ya Chamwino ni miongoni mwa Wilaya saba zinazounda Mkoa wa Dodoma, Makao makuu ya Wilaya ya Chamwino yapo katika Kijiji cha Chamwino kilichopo Kata ya Chamwino, Tarafa ya Chilonwa umbali wa KM 30 kutoka Manispaa ya Dodoma. Wilaya ya Chamwino ina ukubwa wa $Km^2$ 8,056. Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi iliyofanyika mwaka 2012 Wilaya ya Chamwino ilikuwa na idadi ya watu 330,543 kati yao Wanawake ni 171,661 na Wanaume ni 152,882. Wilaya ya Chamwino ina jumla ya Vitongoji 814, Vijiji 107, Kata 36 na Majimbo mawili ya uchaguzi Chilonwa na Mtera.

## II: MAFANIKIO KATIKA UKUSANYAJI WA MAPATO YA WILAYA YA CHAMWINO

Katika kipindi cha miaka miwili cha uongozi wa Mhe: Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt: John Pombe Magufuli Wilaya imeweza kufanikiwa kuboresha vyanzo vyake vya mapato na kutekeleza miradi ya Maendeleo katika Sekta mbalimbali. Katika kuboresha ukusanyaji wa mapato Halmashauri ya Wilaya imeweza kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato kwa kununua na kuimarisha vitu vifuatayo:-

- Halmashauri ya Wilaya ya imenunua Boti ya doria kwa ajili ya kudhibiti uvuvi haramu na ukwepaji wa mapato katika bwawa la Mtera. Boti hii imesaidia kuongeza mapato yatokanayo na uvuvi wa samaki kutoka **Tsh 15,371,500.00** mwaka 2015/2016 hadi **Tsh. 61,674,780.00** mwaka 2016/2017 sawa na ongezeko la asilimia 301.
- Halmashauri ya Wilaya imenunua mashine 50 za kielektroniki za kukusanyia mapato na kuunda timu ya maafisa watano kwa ajili ya kufuatilia mapato yatokanayo na minada. Mkakati huu umesababisha mapato yatokanayo na minada kuongezeka kutoka **Tsh. 209,552,000.00** kwa mwaka 2015/2016 hadi **Tsh. 310,925,500.00** kwa mwaka 2016/2017 sawa na ongezeko la asilimia 48. Aidha, ushuru wa mazao umeongezeka kutoka **Tsh 101,870,500.00** hadi **Tsh 148,577,700.00** sawa na asilimia 46.

**III: MAFANIKIO KATIKA UWEKEZAJI**

Katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Mhe: Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt: John Pombe Magufuli, Wilaya imeandika jumla ya maandiko 10 ya miradi. Maandiko hayo yamewasilishwa kwa wadau/wafadhili ili kuvutia wawekezaji katika Sekta za Viwanda, Kilimo, Mifugo na Ardhi. Maandiko hayo yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama jedwali linavyoonesha:-

| NA | ANDIKO LA MRADI | THAMANI | MATOKEO YA ANDIKO |
|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa kiwanda cha Sukari Kijiji cha Dabalo | 7,500,000,000 | Mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha sukari Kijiji cha Dabalo umefikia hatua ya kusaini mkataba wa awali. Mkataba huo kati Halmashuri na Mwekezaji kampuni ya PURANDARE INDUSTRIES (T) LTD na Bodi ya sukari ilisainiwa tarehe 11 Agosti, 2017 kwa ajili ya utekelezaji. |
| 2 | Mradi wa bwawa la umwagiliaji Kijiji cha Membe | 700,000,000 | Mradi wa bwawa la umwagiliaji Kijiji cha Membe upo katika hatua ya upembuzi yakinifu. Asasi ya LIC imetoa kiasi cha Tsh. 4, 580,000 kwa ajili ya upembuzi yakinifu. |
| 3 | Ujenzi wa kiwanda cha Zabibu Chinangali II | 31,000,000,000 | Mradi wa kiwanda cha zabibu Chinangali II upo katika hatua za awali za utekelezaji ambapo Makubaliano ya awali kati ya Wilaya , GEPF, WCF na Benki ya TIB yalisainiwa tarehe 03/04/2017. Hadi sasa jumla ya Tshs 26,000,000,000 zimeidhinishwa na bodi za na GEPF na WCF na kiasi cha Tshs 5,000,000,000 zilizobaki zitatolewana na benki ya TIB. Ujenzi wa kiwanda hiki |

| NA | ANDIKO LA MRADI | THAMANI | MATOKEO YA ANDIKO |
|---|---|---|---|
| | | | unatarajia kuanza mwezi Aprili 2018 |
| 4 | Ujenzi wa kiwanda cha Maembe Kata ya Huzi | 432,345,000 | Mradi wa kiwanda cha Maembe kata ya Huzi unaotarajiwa kufadhiliwa na Serikali ya Denmark kupitia shirika la LIC kwa sasa upo katika hatua ya kupanua mashamba ya maembe kutoka ekari 200 hadi ekari 700. Tarehe 31/07/2017 Balozi wa Denmak (T) alitembelea mradi huo na kuahidi kutoa Tsh 153,781,000 kwa ajili ya upanuzi wa mashamba. |
| 6 | Ujenzi wa soko la Mazao Kijiji cha Haneti | 385,718,451 | Mradi wa Ujenzi wa soko la mazao Haneti, umefikia hatua ya kufanya upembuzi yakinifu. |
| 7 | Ujenzi wa Kiwanda cha Ngozi Kijiji cha Chalinze Nyama | 82,596,000 | Ujenzi wa kiwanda cha ngozi Kijiji cha Chalinze Nyama andiko limepokelewa kwa ufadhiliwa wa shirika la Local Investment Climate (LIC) |
| 8 | Kuboresha Minada 2 ya Mifugo | 228,860,213.40 | Uboreshaji wa Minada miwili ya mifugo andiko limepokelewa na kukubali kufadhiliwa na shirika la Local Investment Climate (LIC) kwa gharama iliyoandikwa katika andiko |
| 9 | Ujenzi wa kituo cha Biashara na Uwekezaji (One Stop Business Centre) Kijiji cha | 63,000,000 | Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Biashara na Uwekezaji unaendelea na upo katika hatua ya ukamilishaji wa jengo,Ujenzi wa kituo hiki cha uwekezaji kimefadhiliwa na shirika la Local |

| NA | ANDIKO LA MRADI | THAMANI | MATOKEO YA ANDIKO |
|---|---|---|---|
| | Buigiri | | Climate Investment (LIC). Lengo ni kutoa huduma zote za kibiashara katika jengo moja. |
| 10 | Andiko la Mkopo wa fedha katika Benki za CRDB, NMB Plc na mfuko wa Hifadhi ya jamaii GEPF, LAPF kwa ajili ya kulipa fidia ya kutwaa maeneo ili kupima viwanja katika vijiji vya Buigiri na Chamwino. | 3,369,879,449 | Andiko limewasilishwa ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa mapitio na ushauri. Hata hivyo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa imeridhia na kuliwasilisha kwa Katibu Mkuu OR-TAMISEMI kwa ajili ya hatua zaidi. |
| 11 | Andiko la ujenzi wa kiwanda cha ngozi kijiji cha Idifu | 400,000,000 | Andiko limekubaliwa na ujenzi wa kiwanda unaendelea, Ujenzi umefikia hatua ya kupaua. Kiwanda hiki kinajengwa kwa ufadhili wa shirika la ECO - ACT |

**MAFANIKIO YA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTEKELEZWA**

Katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Mhe: Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt: John Pombe Magufuli, Wilaya ya Chamwino imefanikiwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta za Elimu, Afya, Maji, ujenzi na barabara. Miradi hii imegharimu jumla ya Tsh. **16,471,792,643.00** kwa kila sekta kama ifuatavyo:-

## 1: MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA AFYA

Katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Mhe: Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt John Pombe Magufuli jumla ya zahanati 5 ,wodi ya kulaza wagonjwa 1 na nyumba ya mganga 1 zimeweza kujengwa na kukamilika katika vijiji vya Champumba, Mlimwa, Segala, Ndebwe, Manchali "A na Solowu ambapo jumla ya **Tshs 106,000,000.00** zimetumika katika kukamilishaji ujenzi. Wilaya ya Chamwino katika kipindi cha miaka miwili 2015/16 – 2016/17 imefanikiwa kununua dawa, vifaa tiba na vitenganishi kwa gharama ya **Tshs 732,556,514.00**. Aidha katika kipindi cha mwaka 2017/18 Wilaya imepokea **Tshs 900,000,000.00** kutoka Serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya Afya Chamwino na Mpwayungu na utekelezaji wa ujenzi wa mradi huu upo katika hatua ya awali. Zabuni za kupata mafundi zimetangazwa na mafundi wamepatikana. Kwasasa Wilaya inaendelea na taratibu za ununuzi wa vifaa vya ujenzi tayari kwa kuanza ujenzi. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2017/18 Wilaya inaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa zahanati ya Ilangali kwa gharama ya **Tshs 20,000,000.00.**






**2: MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA ELIMU**

***I: ELIMU MSINGI***

Wilaya imeweza kununua madawati 2,000 yenye jumla ya **Tshs 44,800,000.00**, ujenzi wa madarasa 26, Ofisi 9 za walimu, ujenzi wa matundu 26 ya vyoo na nyumba 02 za walimu. Ujenzi wa miundombinu hii ya Shule imejengwa katika shule za msingi Fufu, Chiboli, Mapinduzi, Amani, Majengo Mapya, Nyamalela na Uwanja ambayo imetumia jumla ya **Tshs 482,000,000.00.** Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu hii katika shule za Msingi ni moja ya mafanikio katika kipindi cha miaka miwili ya Mhe: Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania. Hata hivyo miundombinu hii imesaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani na kuweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi kwa walimu ili kuweza kuinua kiwango cha ufaulu kwa shule za Msingi. Katika kipindi cha mwaka 2017/18 Wilaya imetumia **Tshs 132,600,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 6 matundu 12 ya vyoo, madawati 90 meza 3 na viti 3 vya walimu katika shule za msingi Huzi na Mvumi Makulu. Ujenzi katika shule ya Msingi Huzi umekamilia na ujenzi katika shule ya msingi Mvumi makulu upo hatua ya ukamilishaji.

**ELIMU BURE MSINGI**

Katika kipindi cha miaka miwili Wilaya imeweza kutekeleza sera ya Elimu bure kwa kulipa fidia ya ada kwa wanafunzi wote katika shule 119 za Msingi zilizopo Wilaya ya Chamwino, Jumla ya kiasi cha Tshs **1,077,391,272** kimetumika kulipa fidia ya Ada.




***II: ELIMU SEKONDARI***

Katika kipindi cha miaka miwili cha uongozi wa Mhe: Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt: John Pombe Magufuli Wilaya imeweza kujenga maabara 1, madarasa 6 na kununua meza na viti 430, matundu 10 ya vyoo, ujenzi wa mabweni 3, ununuzi wa vitanda double deckers 128, ununuzi wa Magodoro 128, ujenzi wa nyumba 2 za walimu zenye muundo wa 6x1, na ujenzi wa ofisi 1 ya walimu. Ununuzi na ujenzi wa miundombinu hii imefanyika katika shule za

Sekondari Mvumi Misheni, Chamwino, Idifu, Membe na Manzase ambapo jumla ya **Tshs 797,500,000** zimetumika.

**ELIMU BURE**

Katika kipindi cha miaka miwili Wilaya imeweza kutekeleza sera ya Elimu bure kwa kulipa fidia ya ada kwa wanafunzi wote katika shule 27 za sekondari zilizopo Wilaya ya Chamwino, Jumla ya kiasi cha Tshs **524,389,228** kimetumika kulipa fidia ya Ada.



Vyumba vinne vya madarasa shule ya Sekondari Chamwino



Ujenzi wa ofisi ya walimu katika shule ya Sekondari Chamwino

## 3: MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA MAJI

Katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Mhe: Rais John Pombe Magufuli, Wilaya imeweza kuchimba, kusambaza na kujenga visima virefu 17 vya maji hivyo kuongeza huduma ya upatikanaji wa maji safi na salama kufikia asilimia 60% . Ujenzi wa miundombinu hii ya maji imegharimu Tshs **2,524,759,478** Miongoni mwa Vijiji ambavyo vimefanikiwa kujengewa na kusambaza miundombinu ya maji ni pamoja na Fufu, Suli, Chiboli, Manzase, Wilunze, Buigiri, M/Bwawani, Dabalo, Membe, Segala na Chamwino. Hata hivyo upatikanaji wa huduma hii umeweza kusaidia wananchi kutumia muda wao mwingi katika suala la kiuchumi kwani hapo awali huduma hii ilikuwa haipatikani kirahisi wananchi walikuwa wanatembea zaidi ya Km 15 kwa ajili ya kutafuta maji.



Ujenzi wa tank la kusambazia maji katika kijiji cha Suli



Ujenzi wa Kisima Kirefu cha Maji

## 4: MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA UTAWALA

Katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Mhe:Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt: John Magufuli, Wilaya inaendelea na ujenzi wa jengo la Halmashauri na Ofisi moja ya Serikali ya Kijiji Nagulo Mwitikira. Fedha zilizotumika katika awamu ya nne ya ujenzi ni Tsh **446,850,085**. Serikali ya awamu ya tano imetoa jumla ya **Tsh. 1,250,000,000.00** kwa kipindi cha miaka miwili ili kukamilisha ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri. Kiasi kilichobaki cha Tshs **803,149,915** kitatumika kukamilisha ujenzi wa awamu ya nne. Halmashauri ya Wilaya Chamwino inategemea kuhamia katika jengo jipya mwezi Machi 2018. Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la Utawala kutaongeza tija na ufanisi kwa watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino.




## 5: MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA MIFUGO/UVUVI

Katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Mhe: Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt: John Pombe Magufuli, Wilaya ya Chamwino imefanikiwa kununua Injini 1 na kuunda boti kwa gharama ya **Tshs 8,500,000.00** Boti hiyo linatumika kupambana na wavuvi haramu na wanaotorosha samaki na kukwepa kulipa ushuru. Juhudi za kupambana na uvuvi haramu zimefanikiwa kuteketeza nyavu haramu zaidi ya 30 ambazo zilikamatwa na zingine kusalimishwa. Aidha, juhudi zimefanyika katika kuongeza mapato yatokanayo na shughuli za uvuvi. Mapato yatokanayo na uvuvi yameongezeka kutoka **Tsh 15,371,500.**00 mwaka 2015/2016 hadi **Tsh. 61,674,780.00** mwaka 2017/2018.

Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na kusimamia na kutekeleza sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji Mifugo ya mwaka 2010 kifungu cha 12.

Mpaka zoezi linakamilika jumla ya ng’ombe 327,364 walisajiliwa na kupigwa chapa sawa na asilimia 109 ya lengo. Zoezi hili lilifanyika katika vijiji vyote 107 vya Wilaya ya Chamwino. Wafugaji walitakiwa kuchangia gharama za usajili na kupiga chapa kwa kulipa Sh. 500/= kwa kila ng’ombe aliyesajiliwa.



Uundaji wa Boti kwa ajiri ya doria ili kudhibiti uvuvi haramu




## 6: MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA UJENZI WA BARABARA

Katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Mhe:Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt: John Pombe Magufuli Wilaya ya Chamwino imefanikiwa kutengeneza na kuimarisha barabara za Chamwino Ikulu ambapo jumla ya Km 5 zimejengwa kwa gharama ya **Tshs 511,943,202.00** hata hivyo Wilaya imefanya matengenezo ya muda maalumu barabara ya Handali – Chanhumba - Igandu 26 km kwa gharama ya **Tshs 101,338,600.00** na Matengenezo ya muda maalumu barabara ya Nagulo mwitikira - Mpwayungu 15.km kwa gharama ya **Tshs 126,552,050.00**. Aidha Wilaya ya Chamwino

imefanya matengenezo ya kawaida ya barabara yenye urefu wa Km 56, sehemu korofi Km 82 na ujenzi wa Culvate 37. Jumla ya **Tshs 784,710,000.00** zimetumika katika matengenezo hayo.










## 7: MAFANIKI SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII - KITENGO CHA TASAF

Katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Mhe:Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt: John Pombe Magufuli imefanikiwa kulipa fedha kwa kaya 19,132 za walengwa katika vijiji 50 vya Mpango kipindi cha 2015/16

na 2016/17 na jumla ya fedha Tshs **6,588,803,000.00** zimelipwa kwa ajili ya miradi ya nguvu kazi, fedha za masharti na ununuzi wa vifaa vya miradi ya ajira ya muda katika vijiji 50 vya mpango (PWP). Aidha Wilaya kupitia mradi huu wa kunusuru kaya masikini TASA III imeweza kufanikiwa kujenga na kuchimba mabwawa 74, kutengeneza barabara za vitongoji 128, kujenga makinga maji katika vijiji 32 na kuweza kutengeneza manusu duara 88 kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa.




**8: MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA KILIMO NA UMWAGILIAJI**

Katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Mhe:Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt: John Pombe Magufuli Wilaya ya Chamwino kwa kushirikiana na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) na Shirika la Good Neighbors imefanikiwa kujenga miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji katika kijiji cha Suli na Jumla ya hekali 100 zitatumika katika skimu hiyo kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, skimu ya umwagiliaji katika Kijiji cha Suli, imegharimu **Tshs 529,000,000.00** ambapo jumla ya wakulima 120 wanategemea kulima zao la Ufuta, Alizeti, Mahindi na Mtama kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji kwa mwaka mzima. Hata hivyo katika Kipindi cha 2017/18 ujenzi unaendelea wa Skimu za umwagilaji katika vijiji vya Fufu na Chiboli ambapo jumla ya **Tshs 518,000,000.00** zimetumika katika ujenzi wa Skimu hizo na ujenzi unategemea kukamilika mwezi Aprili 2018. Jumla ya wakulima 120

wanategemea kulima zao la Ufuta, Alizeti, Mahindi na Mtama kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji kwa mwaka mzima. Hata hivyo Katika kipindi hiki Wilaya imefanikiwa kujenga vituo vinne vya Kilimo (Agriculture resource Centres) katika kata za Buigiri, Haneti, M/barabarani na Msanga. Dhumuni la kujenga vituo hivi ni kutoa huduma za karibu za kilimo na wakulima kuweza kujifunza utaalam wa kilimo kutoka kwa wataalam waliopo Wilayani.Mradi huu umegharimu jumla ya **Tshs 218,825,036.00** na miradi yote imekamilika.



Ujenzi wa skimu ya umwagiliaji katika Kijijij cha Suli




Naomba kuwasilisha,

VUMILIA JUSTINE NYAMOGA
MKUU WA WILAYA
**CHAMWINO**